



ISSN 0856-6976

**MUHTASARI WA TAMKO
LA SERA YA FEDHA**

2017/18

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2017



ISSN 0856-6976

**MUHTASARI WA TAMKO
LA SERA YA FEDHA
2017/18**

**GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2017



Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, Benki Kuu inatoa Tamko la Sera ya Fedha linaloweka bayana mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2017/18. Tamko hili linajumuisha mapitio ya utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2016/17 na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2017/18. Tamko hili pia linaelezea msingi wa malengo hayo na hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ili kuyafikia.

Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Aprili 2017, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2016 ulikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2015. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumechangiwa zaidi na ukuaji hafifu katika mataifa yaliyoendelea kiuchumi, pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara. Ukuaji hafifu wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea ulitokana na kushuka kwa mahitaji katika soko la dunia pamoja na kasi ndogo ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji. Kwa upande mwingine ukuaji hafifu wa uchumi wa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara ulitokana kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, pamoja na ukame.

Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 3.5 mwaka 2017 na asilimia 3.6 mwaka 2018, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika mataifa yaliyoendelea na yale yanayoibukia kiuchumi. Mwaka 2017 na 2018, ukuaji wa uchumi katika



mataifa yaliyoendelea unatarajiwa kufikia asilimia 2.0, wakati ukuaji wa uchumi katika mataifa yanayoibukia unakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka 2017 na asilimia 4.8 kwa mwaka 2018. Ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara unatarajiwa kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 2.6 kwa mwaka 2017 na asilimia 3.5 kwa mwaka 2018, kutoka asilimia 1.4 mwaka 2016. Hii ni kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na kuimarika kwa matumizi na mahitaji binafsi.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Aprili 2017, kasi ya mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi iliongezeka isipokua China na India. Mfumuko wa bei uliongezeka nchini Marekani, nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya, Japan na Uingereza kutokana hasa na kupanda kwa bei za mafuta na nishati. Kupungua kwa mfumuko wa bei nchini China na India kulitokana na ongezeko dogo la bei za vyakula na vinywaji. Wakati huo huo, mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Afrika ya Mashariki uliongezeka kutokana na kupanda kwa bei za vyakula, wakati mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Kusini mwa Afrika ulipungua kutokana na kupungua kwa bei za vyakula.

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili 2017, mfumuko wa bei unatarajiwa kuongezeka katika mataifa yaliyoendelea kufikia wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2017, kutoka asilimia 0.8 mwaka 2016; wakati kwa mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea kiuchumi mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 4.7 kutoka asilimia 4.4. Ongezeko hili litatokana zaidi na matarajio ya kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.



Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Tanzania Bara

Uchumi umeendelea kuimarika ambapo pato la taifa limekua kwa asilimia 7.0 mwaka 2016, sawa na ukuaji uliofikiwa mwaka 2015 na 2014. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kimechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuendelea kuimarika kwa uwekezaji katika miundombinu, kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme, kukua kwa uwekezaji katika utoaji wa huduma za simu za mikononi na mtandao, pamoja na bei ya mafuta kuendelea kuwa chini katika soko la dunia. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na ujenzi (asilimia 13.0), mawasiliano (asilimia 13.0), usafirishaji na uhifadhi (asilimia 11.8), madini (asilimia 11.5), na fedha na bima (asilimia 10.7). Shughuli za ujenzi zimeendelea kuongoza kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la taifa kwa miaka mitatu mfululizo, ambapo mwaka 2016 zilichangia asilimia 20.3 kutoka asilimia 23.9 katika mwaka 2015. Shughuli nyingine zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa pato la taifa ni pamoja na usafirishaji na uhifadhi (asilimia 10.7), biashara ya jumla na rejareja (asilimia 9.9) na mawasiliano (asilimia 8.3).

Uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa imara katika mwaka 2017, ukikadiriwa kukua kwa zaidi ya asilimia 7, kutokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia, kuendelea kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme, na jitihada za Serikali katika kuwekeza katika miundombinu, na sera ya kuendeleza viwanda nchini chini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.



Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, mfumuko wa bei uliendelea kubakia katika tarakimu moja. Hali hii ilichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na ya kibajeti, pamoja na bei ya mafuta kuendelea kuwa ya chini katika soko la dunia, kuimarika kwa uzalishaji wa nishati ya umeme nchini na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni za mataifa makubwa. Katika kipindi hicho, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 6.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) ulikuwa wa wastani wa asilimia 2.4 katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Aprili 2017, sawa na kiwango kilichofikiwa kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja ukiendana na lengo la asilimia 5.0. Hali hii itachangiwa na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula, utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na kibajeti, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati nchini, bei ya mafuta kuendelea kuwa ya chini katika soko la dunia, na kuendelea kwa utulivu wa thamani ya shilingi.

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yameendelea kuongezeka na kufikia shilingi bilioni 13,090.6, sawa na ongezeko la asilimia 18.6 zaidi ya mapato yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16. Katika kipindi hicho, kiasi cha fedha halisi (*net issuance*) ya bajeti zilizopatikana kutokana na uuzaji wa dhamana na hati fungani za serikali kilikuwa shilingi bilioni 752.5, wakati fedha za wahisani zilikuwa sawa na shilingi bilioni 675.4. Jumla ya matumizi yaliyopitia katika akaunti za serikali zilizoko Benki Kuu



yalifikia shilingi bilioni 14,385.1; ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 10,866.2, na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,518.9.

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ilipungua kwa asilimia 51.6 na kufikia dola za Marekani milioni 1,096.4, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,263.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Kupungua huko kwa nakisi ya urari wa biashara kulitokana zaidi na kupungua kwa thamani ya uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 3,870.3 mwishoni mwa mwezi Juni 2016 hadi kufikia dola za Marekani milioni 4,413.6 mwishoni mwa mwezi Aprili 2017, ambazo zinatoshwa kuagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.3. Wakati huo huo, rasilimali za fedha za kigeni za mabanki ya biashara zilikuwa dola za Marekani milioni 657.4, wakati amana za fedha za kigeni zilizohifadhiwa na wakazi wa Tanzania katika benki za biashara nchini zikiwa jumla ya dola za Marekani milioni 2,691.9. Nakisi ya urari wa biashara inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 5.0 ya pato la taifa ifikapo mwisho wa mwaka 2016/17, ikilinganishwa na asilimia 6.5 ya pato la taifa mwaka 2015/16, kutokana na matarajio ya kuimarika kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Deni la nje limeendelea kuongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 17,802.6 mwishoni mwa mwezi Aprili 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.4 kutoka dola za Marekani milioni 17,222.8 mwezi Juni 2016. Ongezeko hili limetokana na mikopo mipya pamoja na malimbikizo ya malipo ya riba.



Katika deni hilo la nje, asilimia 80.3 ni deni la serikali na taasisi za umma. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la nje la Taifa yaliyofanyika mwezi Novemba 2016, yanaonesha kuwa thamani halisi ya deni la nje ikilinganishwa na Pato halisi la Taifa ni asilimia 19.9, ambayo ni chini ya ukomo uliowekwa kimataifa wa kiwango cha uhimilivu wa deni la nje cha asilimia 40.0, ikidhihirisha kwamba deni la nje la Taifa bado ni himilivu. Deni la ndani liliongezeka kwa asilimia 11.1 na kufikia shilingi bilioni 11,132.3 mwishoni mwa mwezi Aprili 2017 kutoka shilingi bilioni 10,012.8 mwezi Juni 2016. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kukopa kupitia dhamana za serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya serikali kwa mwaka 2016/17.

Katika mwaka ulioishia mwezi Aprili 2017, sekta ya kibenki imeendelea kukua kwa kuanzishwa kwa taasisi mpya katika biashara ya kibenki, na kuendelea kuenea kwa huduma za benki za biashara sehemu mbalimbali nchini. Kujumla, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Uwiano wa mitaji ya mabanki ikilinganishwa na rasilimali zao ulifikia asilimia 19.0 mwezi Aprili 2017, ukiwa juu ya kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0, na asilimia 17.8 iliyokuwa imefikiwa mwezi Aprili 2016. Pia, hali ya ukwasi wa mabanki kujumla imeendelea kubakia katika kiwango cha juu na kufikia asilimia 37.7, ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20, na asilimia 37.0 mwezi Aprili 2016. Aidha, ubora wa rasilimali za mabanki ulipungua kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu kufikia asilimia 10.8 mwezi Aprili 2017 kutoka asilimia 8.2 mwezi Aprili 2016.



Benki Kuu imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa taasisi za fedha kwa kutoa kanuni na miongozo ya kisheria katika kusimamia sekta ya fedha kwa dhati. Aidha, imeziagiza benki zote ambazo zina kiwango cha juu cha mikopo chechefu zaidi ya asilimia 5.0 kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa ubora wa rasilimali zao unaimarika na kubakia ndani ya kiwango cha asilimia 5.0 kinachotakiwa na Benki Kuu. Pia Benki Kuu imeendelea kusisitizia mabanki kutumia taarifa za wakopaji katika mfumo wa kuhifadhi na kutoa taarifa za wakopaji (Credit Reference System) ili kusaidia kupunguza idadi ya mikopo chechefu. Benki Kuu imeagiza mabanki ya biashara kuendelea na zoezi la kuimarisha mitaji yake kwa asilimia 2.5 (Capital Conservation Buffer) linalotarajiwa kuanza kutekelezwa rasmi mwezi Agosti 2017.

Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi huku miamala inayotumia simu za mikononi ikiongezeka na kufikia milioni 1,444.6 yenye thamani ya shilingi bilioni 49,997.1 katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Aprili 2017, ikilinganishwa na miamala milioni 1,217.7 yenye thamani ya shilingi bilioni 43,867.9 katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016. Idadi ya Watanzania waliokuwa watumiaji hai wa mfumo wa malipo kwa njia ya simu za mikononi ilifikia milioni 17.3 mwezi Aprili 2017.

Zanzibar

Katika mwaka 2016, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.8, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.5 mwaka 2015. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na uchimbaji madini na mawe (asilimia 18.8), ujenzi (asilimia 11.3) na shughuli za sanaa na burudani (asilimia 9.8).



Mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 7.1 mwaka ulioishia mwezi Aprili 2017, kutoka asilimia 10.1 mwezi Aprili 2016. Upunguaji huu ulitokana na kushuka kwa bei za vyakula, mahoteli na migahawa, mavazi na viatu. Aidha, kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kuendelea kubakia ndani ya tarakimu moja katika mwaka wa fedha 2017/18, kutokana na matarajio ya kuendelea kupungua kwa bei za vyakula na mafuta.

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, jumla ya mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yalifikia shilingi bilioni 476.7. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 445.9, na mapato ya nje yalikuwa shilling bilioni 30.8. Jumla ya matumizi ya serikali ilikuwa shilingi bilioni 482.5; kati ya hizo, matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 382.3, wakati matumizi ya maendeleo yalikuwa ni shilingi bilioni 100.2. Katika kipindi hicho, nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kutoka nje ilikuwa shilling bilioni 5.9.

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje uliimarika na kufikia ziada ya dola za Marekani milioni 38.3 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 10.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16. Hali hii ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa pamoja na kuongezeka kwa misaada kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi 2017, deni la Zanzibar lilipungua na kufikia shilingi bilioni 377.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 385.7 mwishoni mwa mwezi Juni 2016. Deni la nje liliongezeka kutoka shilingi bilioni 268.8 mwezi Juni 2016 hadi shilingi bilioni 270.2 mwezi Machi 2017, ambalo ni sawa na asilimia 71.7 ya jumla ya deni lote la Zanzibar. Deni la ndani lilipungua kutoka shilingi bilioni 117.0 mwezi Juni 2016 hadi shilingi bilioni 106.8 mwishoni mwa mwezi Machi 2017.



Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2016/17

Malengo ya Sera ya Fedha

Ili kufikia malengo ya serikali ya uchumi jumla kwa mwaka 2016/17, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutimiza malengo yafuatayo:

- i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim usiozidi asilimia 12.0;
- ii. Ukuaji wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 12.3
- iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 12.5; na
- iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0).

Utekelezaji wa Sera ya Fedha

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, hali ya ukwasi katika mabanki ilikuwa ilikuwa chini hususan katika nusu ya kwanza ya mwaka 2016/17. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa fedha za misaada kwa ajili ya bajeti kutoka nje ya nchi na uhamishaji wa amana za taasisi za umma kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu. Kupungua kwa ukwasi kulichangia ukuaji mdogo wa fedha kwa tafsiri pana kufikia asilimia 3.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili 2017, ikilinganishwa na asilimia 12.9 katika mwaka ulioishia mwezi Aprili 2016. Pia mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 19.3. Aidha, kufuatia kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia kwenye mifumo ya malipo na kuendelea kuimarika kwa utoaji wa huduma za kifedha nchini, kumesaidia kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa



fedha (*money multiplier and velocity of money circulation*) hali ambayo imesaidia kupunguza athari za kasi ndogo ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwenye uchumi.

Kufuatia mwenendo wa kupungua kwa kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha, Benki Kuu katika kutekeleza sera ya fedha ilichukua hatua za makusudi za kuongeza ukwasi kupitia zana mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabanki ya biashara, kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soko la jumla la mabanki, kushusha riba (*discount rate*) kutoka asilimia 16 hadi asilimia 12 mwezi Machi 2017, na kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara (*Statutory Minimum Reserve Requirement*) toka asilimia 10.0 hadi asilimia 8.0 mwezi Aprili 2017. Hatua hizi zimesaidia sana kuboresha hali ya ukwasi kwenye benki za biashara na kusaidia riba katika soko la fedha baina ya mabanki (*interbank cash market (IBCM) interest rate*) kupungua kutoka asilimia 12.76 mwezi Juni 2016 hadi asilimia 7.19 mwezi Aprili 2017.

Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017, thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu, kutokana na usimamizi na utekelezaji wa sera nzuri ya fedha, usimamizi thabiti wa mapato na matumizi ya Serikali, pamoja na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje.



Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18, Serikali zitaendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II 2016/17 – 2020/21*) pamoja na Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA III 2015-20) inayolenga kuendeleza jitihada za kuweka misingi imara ya shughuli za viwanda na kukuza uchumi. Katika mwaka 2017/18, pato la taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2, kutokana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2017 na asilimia 7.3 kwa mwaka 2018. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika kiwango cha tarakimu moja, wakati nakisi ya bajeti ya serikali inatarajiwa kuwa asilimia 3.8 ya pato la taifa.

Kwa upande wa Zanzibar, pato la taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.1, kutokana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2017 na asilimia 7.0 kwa mwaka 2018. Nakisi ya bajeti ya serikali ya Zanzibar inatarajiwa kuwa asilimia 1.1 ya pato la taifa.

Ili kufikia malengo ya serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2017/18, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

- i. Ukuaji wa fedha taslim usiozidi asilimia 12.6;
- ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi wa asilimia 12.5;
- iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 14; na
- iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.



Katika mwaka 2017/18, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuhakikisha kuwa hali ya ukwasi inaendana na malengo ya ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei. Hali ya ukwasi katika benki za biashara itaendelea kuimarika kufuatia hatua za sera ya fedha zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2016/17. Hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu zinatarajiwa pia kuongeza uwezo wa benki za biashara kutoa mikopo ya riba nafuu kwa sekta binafsi na hivyo kusaidia kuongeza uzalishaji na shughuli za kiuchumi. Benki Kuu itendelea kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa amana za ziada (*clearing balances*) za benki za biashara zinazohifadhiwa Benki Kuu kwa ajili ya shughui za kila siku za benki na kutumia zana zake za utekelezaji wa sera ya fedha ili kuhakikisha kwamba ukwasi unabakia kwenye kiwango kinachoendana na utulivu wa riba za muda mfupi, na kuhakikisha mfumuko wa bei unabakia ndani ya lengo la asimilia tano.

Aidha, Benki Kuu itaendelea kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha na kutumia riba kama kiashiria cha mwelekeo wa sera ya fedha. Matumizi ya riba pia ni utekelezaji wa moja kati ya malengo ya kurazinisha sera za fedha chini ya Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hatua zitakazoendelea kuchukuliwa kabla ya kutumia riba ni pamoja na kuboresha mfumo wa mabanki kukopeshana kwa kuufanya uwe wa kielektroniki ili kuongeza ufanisi na uwazi baina ya mabanki (*electronic platform for interbank cash market operations*), pamoja na kufanya mapitio ya mfumo wa dhamana (*review of the collateral framework*) na kuendelea kukuza ufanisi katika mfumo ya malipo nchini. Hatua nyingine ni pamoja na kutumia mfumo wa maoteo (*Forecasting and Policy Analysis System (FPAS)*) katika uchambuzi na utekelezaji wa sera



ya fedha na kuweka miongozo itakayotumiwa na benki za biashara katika kutekeleza sera ya fedha pamoja na kuongeza mawasiliano.

Katika mwaka 2017/18, kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni katika soko la jumla la mabanki (*interbank foreign exchange market*) kitaendelea kuongozwa na nguvu ya soko. Aidha, Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa ajili ya kuhakikisha kiwango cha ujazi wa fedha kinawiana na mahitaji halisi ya uchumi na kuhakikisha kuwa thamani ya shilingi inaendelea kuwa tulivu. Ushiriki wa Benki Kuu katika soko la fedha za kigeni utaendelea kuhakikisha kwamba kiwango cha akiba za fedha za kigeni kinabakia ndani ya lengo.

Matarajio na Hitimisho

Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kuwa imara katika mwaka 2017/18 kutokana na Serikali kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan, FYDP II 2016/17 – 2020/21*) na Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA III 2015-20), pamoja na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa mataifa yaliyoendelea, na yale yanayoibukia na yanayoendelea kukua kiuchumi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya tarakimu moja katika mwaka 2017/18 kutokana na matarajio ya bei ya mafuta kuendelea kubakia chini katika soko la dunia; utulivu wa thamani ya shilingi; na kuendelea kupatikana kwa chakula nchini. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua tahadhari na ikibidi kuchukua hatua za ziada za kisera katika kudhibiti ongezeko la mfumuko wa bei endapo litatokea.



Benki Kuu itaendelea kuboresha masoko ya fedha na sekta ya fedha kwa ujumla ili kutatua changamoto zilizopo. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera yake ya fedha katika kusimamia ukwasi kulingana na mahitaji halisi ya kiuchumi.

Benki Kuu ina imani kwamba malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2017/18 yatafikiwa kwa ushirikiano na sera ya kibajeti. Hali hii itachangiwa pia na kuimarika kwa uchumi mpana na hali ya kifedha duniani, pamoja na usimamizi mzuri wa mapato na matumizi ya serikali.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: <http://www.bot.go.tz>

Kimepigwa Chapa na Identity Promotion Ltd